**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI TUMAINI – IRAMBA MKOA WA SINGIDA

**Tarehe 23/04/2024**



Scanned with CamScanner

**OFISI YA RAIS,**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI TUMAINI**

S.L.P 533 KINAMPANDA,
SINGIDA.
23/04/2024.

Mkuu wa Shule: Severina Frank Chuwa
Simu: **0769184185/ 0657971377/0783996523**
Barua pepe: tumainisecondaryschool1969@gmai.com.
Makamu mkuu wa shule: **0755002094/0759455023**
Matron: **0764883101**
Instagram: **tumainisecondaryschool**

NDG MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI: ……………………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TUMAINI, HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA MKOA WA SINGIDA**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule ya sekondari Tumaini iliyopo Wilaya ya Iramba katika Mkoa wa Singida mwaka 2024 katika Tahasusi ya HGE/HGK/HGL/HK/PCB/HGFa na HGLi. **KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI TUMAINI**.
2. Shule iko kilometa 70 kutoka Singida mjini.
   Kama utapanda basi la moja kwa moja toka Dar es salaam, Moshi, Arusha N.K yaani mabasi yote yenye uelekeo wa Kwenda Mwanza Shinyanga (barabara ya kati) atashuka kituo kinachoitwa **KITUSHA**, na hapo atapanda boda boda au gari ndogo aina ya HIACE ni umbali wa kilomita nane (8KM) mpaka kufika Shuleni.
3. Kutoka Singida mjini atapanda mabasi katika kituo cha mabasi MSUFINI au JENGO LA CCM, hapo utakuta magari aina ya HIACE; ambayo huondoka Singida mjini kati ya saa 6:30 na saa 7:00 mchana kila siku Kwenda kijiji cha Kinampanda ilipo shule. Nauli ni shilingi elfu tano kama hakutakuwa na mabadiliko yeyote. Endapo atachelewa muda huo apande gari yeyote inayoenda kiomboi au Igunga katika vituo hivyo vya mabasi na ashuke katika kituo cha Magari KITUSHA.
4. Endapo mwanao atapanda mabasi ya kutoka Tabora, Nzega, Kahama au Mwanza Kwenda Arusha, Dar es salaam ashukie sehemu iitwayo **Kitusha** kilomita chache toka kituo cha mabasi cha Misigiri.



Scanned with CamScanner

Kutoka **KITUSHA** kuna umbali wa kilomita nane (8) mpaka shuleni, hivyo atakodisha pikipiki mpaka shuleni au atasubiri mabasi aina ya HIACE yatokayo Singida mjini kuelekea kijiji cha Kinampanda ilipo shule.

5. Muhula wa masomo utaanza **1/7/2024** kama ilivyotangazwa kwenye vyombo vya Habari na Wizara inayoshughulikia masuala ya Elimu.
   Aidha una muda mrefu wa kumuandaa mtoto hakuna sababu ya kuchelewa kuripoti shule! Ninasisitiza mwanafunzi afike shuleni mapema tarehe husika muda wa kuripoti ni kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na moja na nusu jioni. Kama kuna dharura tumia namba za shule kuutarifu uongozi.

**MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 SARE YA SHULE

a) Sare ya shule ni sketi ya Blue Bahari (light blue) kitambaa Kizito cha suti grade 1, sketi mbili (2), mshono wa rinda bapa (rinda box) mbele na nyuma, sketi iwe ndefu mpaka chini (juu kidogo ya viatu)
b) Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
c) Wanafunzi wanaovaa hijabu (kijuba) iwe nyeupe na ndefu kufika usawa wa nyonga, na hijabu zote ziwe za kitambaa cheupe aina ya babi au halua (sio kitambaa cha mpira au aina nyingine)
d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, Jozi mbili (2)
e) Sare ya michezo ni bukta na T-shirt rangi ya blue, raba rangi nyeupe (jozi moja) na traki suti rangi ya kijivu (jozi moja)
f) Soksi nyeupe kuanzia jozi mbili
g) Sweta la **blue Bahari** yenye shepu ya V mbele – shingoni
h) Nguo za kushindia (shamba dress) sketi nyeusi moja au mbili marinda ya kupanga (mbele marinda nane au saba na nyuma vivyo hivyo) jumla marinda 16 au 14, iwe ndefu mpaka chini kama sketi ya darasani.
i) Aje na tisheti rangi ya kijivu nzito aina ya form six yenye kola kama picha inavyoonekana hapo chini AU aje na Tsh.30,000/ kwa tisheti mbili ambazo zitapatikana shuleni.
j) Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa isipokuwa aje na kanga/vitenge jozi moja tu, atatumia wakati wa kuoga.
k) Aidha Tumaini Sekondari kuna baridi, hivyo mwanafunzi anaweza kununua pull neck (sweta la kaba shingo) NYEUPE ya kuvalia ndani ya shati la shule.



Scanned with CamScanner

**2:2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo:**

i. Madaftari makubwa (counter book quire 4) madaftari nane na madaftari ya msomi madogo 8 kwa ajili ya majaribio ya ndani.
ii. **Ream (A4)** Mbili (2) kwa ajili ya shughuli za Kitaaluma.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Dissection Kit **ILIYOKAMILIKA** na Scientific Calculator kwa wanafunzi wanaosoma sayansi (PCB)
v. Godoro la sponji futi 2.5 inch 4 na mto wa kulalia
vi. Mashuka Jozi 2 light blue na foronya zake, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*nyeupe);*
vii. Nguo za ndani za kutosha na taulo za kike za kutosha
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na dumu la lita tano la kuhifadhia maji ya kunywa
x. Jembe moja lenye mpini na ufagio mmoja mlaini (soft broom) na chelewa kwa kila mwanafunzi.
xi. Pamoja na vifaa tajwa (number i-xi), tahasusi zifuatazo wataleta vifaa hivi kwa mchanganuo ufuatao:
    - HKL: Dawa ya chooni aina ya ARO, kwanja moja .
    - HGL: Ufagio wa kukaushia maji (squizer) na ARO
    - HGK: Ufagio mgumu wa kusugulia sakafu na ufagio wa kukaushia maji (squizer)
    - HGE: panga moja,na ARO
    - PCB: Dawa ya chooni aina ya ARO na kwanja.
    - HGFa na HGLi.,watering cane na kwanja moja
    - NB. Kila mwanafunzi wa Comb za PCB, HGE, HGK, HGL, HGFa na HGLi anatakiwa aje na rimu moja ya graph paper.

xii. **Kila mwanafunzi aje na BIMA YA AFYA**; kama hana bima ya afya aje na shilingi 6,000/= kwa ajili ya bima ndogo au shilingi 50,400/= kwa ajili ya Bima kubwa.

**2:3 Michango ya uendeshaji wa shule.**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuchangia Tsh. 80,000/= kwa ajili ya uendeshaji wa shule. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **50601100179 – Tumaini Secondary school Recurrent A/C – NMB –** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye Bank pay in slip) aje nayo anaporipoti shule

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**



Scanned with CamScanner

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**



Scanned with CamScanner

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi wa mali za shule, mali z watumishi za jamii na mali za wanafunzi wengine;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wotewawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
NB: Tumaini Sekondari wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

KARIBU SANA TUMAINI SEKONDARI! **KWETU SISI ELIMU NI USHINDI!**



Scanned with CamScanner

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI TUMAINI
S.L.P. 533-KINAMPANDA

.............................................

**SEVERINA FRANK CHUWA**
**MKUU WA SHULE**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOTAJWA MWANZO WA MAELEKEZO HAYA.**

PICHA YA TISHETI ZA KUSHINDIA








Scanned with CamScanner

# OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# SHULE YA SEKONDARI TUMAINI.

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA MWANAFUNZI

| Picha Ya mwanafunzi |
|---|

A. **Habari za mwanafunzi:**

i. Jina kamili…………………………………………………………………………
ii. Tarehe ya kuzaliwa…………………………Wilaya…………………………
iii. Dini………………………Dhehebu…………………………………………

**Mahali atakapokuwa anaenda likizoni:**

i. Jina…………………………Uhusianao…………….Mahali…………….
ii. Jina…………………………Uhusiano……………..Mahali…………….

**Kukubali nafasi:**

Mimi……………………………………nimeona maelekezo ya kujiunga na shule ya Sekondari Tumaini. Nakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na kutii sheria za shule. Nitakapokuwa shuleni, nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kusoma kwa bidii na kuchapa kazi za mikono kwa bidii ili kutimiza lengo la kupata elimu katika ujumla wake.

**Saini……………………….Tarehe…………………………………………………**

| Picha Ya Mzazi/mlezi |
|---|

B. **Habari za Mzazi/Mlezi**

i. Jina kamili…………………………………………………………………
ii. Yeye ni mzazi au mlezi………………………………………………………
iii. Uhusiano uliopo na mwanafunzi……………………………………………
iv. Kazi yake…………………………………………………………………
v. Anwani ya kazini…………………………………………………………
vi. Namba ya simu……………………………………………………………
vii. Anwani ya nyumbani…………………………………………………………
viii. Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi:
Nimehakikisha maelekezo na maagizo yameeleweka na mtoto wnagu atafuata sheria na taratibu zote za shule ya sekondari Tumaini.

**Jina…………………………………….Saini……………………Tarehe………………**

<u>**FORM B**</u>:

Scanned with CamScanner

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

PART A:

TO: The Medical Officer
.................................
.................................
.................................

FROM: The Headmistress,
Tumaini Sec. School,
P.O Box 533,
Kinampanda, IRAMBA- SINGIDA.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI TUMAINI
S.L.P. 533-KINAMPANDA

NAME OF THE STUDENT...............................................................................

Please examine the above named person as to her fitness for re-engagement as a student in our school.

Signature ...........................

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI TUMAINI
S.L.P. 533-KINAMPANDA

PART B: MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by Medical Officer)

I have examined the above named student and consider that she is
.........................................................................................................
.........................................................................................................
.........................................................................................................

**Date**......................................... **Signature** ..........................................................

**Station**......................................... **Designation** ................................................

Scanned with CamScanner